Tarehe ya kuanza kutumika: **Tarehe 4 Februari, 2026**

HOWARD CENTER
Help is here.
***Msaada uko** hapa*

# Ilani ya Utekelezaji ya Faragha

**Ilani hii inafafanua jinsi taarifa yako ya matibabu inavyoweza kutumiwa na kutolewa na jinsi unavyoweza kupata taarifa hii.**
**Tafadhali ipitie kwa uangalifu.**

Ukiwa na maswali yoyote kuhusu ilani hii, tafadhali wasiliana na Afisa wa Faragha wa Howard Centerkwa (802) 488-6900

## WATAKAOFUATA ILANI HII

Ilani hii inafafanua utekelezaji wetu na wa:

- Mtaalam yeyote wa utunzaji wa afya aliyeidhinishwa kuingiza maelezo kwenye kumbukumbu yako ya afya.
- Vitengo na programu zote za Howard Center.
- Mtu yeyote wa kujitolea tunayemruhusu kukusaidia unapopata huduma kutoka Howard Center.
- Waajiriwa wote, watumishi na wafanyakazi wengine.
- Taasisi, maeneo na sehemu zote za Howard Center zinafuata masharti ya ilani hii. Watumishi katika taasisi, maeneo na sehemu hizi wanaweza kupeana taarifa hizi za afya kwa ajili ya matibabu, malipo au uendeshaji kama ilivyofafanuliwa katika ilani hii.

## AHADI YETU KUHUSIANA NA TAARIFA YA AFYA

**Tunafahamu kuwa taarifa ya afya inayokuhusu wewe na afya yako ni siri. Tumejidhatiti kulinda faragha na tarifa yako ya afya.** Tunaunda kumbukumbu ya uangalizi na huduma unazopata kwenye shirika. Tunahitaji kumbukumbu hii ili kukupatia uangalizi bora na kuzingatia mahitaji muhimu ya sheria. Ilani hii inatekelezwa kwa kumbukumbu zote za uangalizi wako zilizotayarishwa na shirika, iwapo zimetengenezwa na mfanyakazi wa shirika au daktari wako binafsi. Huenda daktari wako binafsi akawa na sera au ilani tofauti kulingana na matumizi na utoaji wa tarifa yako ya afya iliyoandaliwa kwenye ofisi au au kliniki ya daktari.

Ilani hii itakuarifu kuhusu njia ambazo tunaweza kutumia na utoaji tarifa ya afya inayokuhusu. Pia tunafafanua haki zako na wajibu mwingine tulio nao kulinagana na matumizi na utoaji tarifa ya afya.

Tunahitajika kisheria:

- Kuhakikisha kuwa taarifa ya afya inayokutambulisha imewekwa faragha;
- Kukupa ilani hii ya shughuli zetu za kisheria na mazoea ya faragha kwa kuzingatia maelezo ya afya yanayokuhusu;
- Kufuata masharti ya ilani yanayotumika sasa;

- Kukuarifu kufuatia ukiukaji wa maelezo ya afya yasiyolindwa kwa usalama; na
- Kuzingatia sheria yoyote ya taifa ambayo ni thabiti zaidi au hukutolea haki kubwa kuliko Ilani hii.

JINSI TUNAVYOWEZA KUTUMIA NA KUFICHUA MAELEZO YA AFYA YANAYOKUHUSU

Howard Center hutoa usaidizi na huduma ili kushughulikia afya ya akili, matumizi ya dawa za kulevya na mahitaji ya ukuaji.

Una haki ya kuidhinisha programu yetu kutumia na kufichua rekodi zako za matibabu ya ugonjwa wa matumizi ya dawa kwa madhumuni ya matibabu yako, malipo, na shughuli za utunzaji wa afya, kulingana na HIPAA. Ukishatoa ridhaa hii, rekodi hizi zinaweza kushirikiwa na watoa huduma wako wa matibabu, mipango ya afya, walipaji wengine, na wale wanaosaidia kuendesha mpango huu, na zinaweza kufichuliwa zaidi kama inavyoruhusiwa na sheria za HIPAA.

Ukitupa ruhusa ya kushiriki rekodi zako za matibabu ya ugonjwa wa matumizi ya dawa kwa ajili ya huduma yako, malipo, au shughuli za afya, mtoa huduma au mpango wowote wa afya anayepokea rekodi zako si lazima azitenganishe na taarifa zako nyingine za afya. Si lazima kuweka rekodi hizi tofauti. Maelezo yako ya ugonjwa wa matumizi ya dawa yanaweza kuwa sehemu ya rekodi yako ya kawaida ya matibabu.

Rekodi zako za matibabu ya ugonjwa wa matumizi ya dawa haziwezi kutumika au kufichuliwa katika mashauri ya kisheria dhidi yako bila ridhaa yako iliyoandikwa au amri mahususi ya mahakama. Unaweza kubatilisha ridhaa yako wakati wowote kwa maandishi, lakini hii haitatumika kwa ufumbuzi ambao tayari umetolewa kwa kutegemea ridhaa yako.

Kategoria zifuatazo zinafafanua njia tofauti tunazotumia na kufichua maelezo ya afya. Kwa kila kategoria ya matumizi na ufichuzi tutafafanua tunachokimaanisha na kujaribu kutoa baadhi ya mifano. Sio matumizi na ufichuzi wote katika kategoria utaorodheshwa.

**Kwa Matibabu**. Tunaweza kutumia au kufichua maelezo ya afya kukuhusu ili kukutolea matibabu au huduma. Hii ni pamoja na uwezekano wa kushiriki maelezo kukuhusu na madaktari, wauguzi, watabibu, wasimamizi wa kesi, wafanyakazi wanafunzi au wafanyakazi wa uwakala mwingine, au kwa watoa huduma walio nje ya uwakala wanaohusika katika utunzaji wako kama vile PCP wako, daktari wa meno, n.k. Kwa mfano, huenda mtabibu anakutibu tatizo la kiakili au matumizi ya dawa za kulevya na angependa kuzungumza na madaktari wa akili, au mtabibu mwingine, aliyehitimu katika mafunzo maalum katika nyanja mahsusiya utunzaji. Pia tunaweza kufichua maelezo kukuhusu kwa watu walio nje ya uwakala wanaohusishwa katika utunzaji wako wa afya.

Ubadilishanaji Kielektroniki wa Maelezo Yako ya Afya-Katika baadhi ya matukio, tunaweza kuhamisha maelezo kukuhusu kieletroniki kwa watoa huduma wengine wa afya wanaokutibu au kwenye mpango wa bima unaotoamalipo kwa matibabu yako. Pia maelezo ya afya kukuhusu yanaweza kupatikana kupitia Ubadilishanaji wa Maelezo ya Afya ya Vermont (“VHIE”). VHIE ni mtandao wa tarifa za afya ambao umeteuliwa na jimbo ambao unaoendeshwa na Vermont Information Technology Leaders, Inc. (“VITL”). Mtoa huduma za afya anayekutibu anaweza kupata taarifa zako za afya kupitia VHIE, isipokuwa kama unahitaji matibabu ya dharura. Kwa tarifa kuhusu VHIE, tazama www.vitl.net.

**Kwa Malipo**. Tunaweza kutumia na kufichua maelezo ya afya kukuhusu ili matibabu na huduma unazopokea katika uwakala ziweze kuidhinishwa na, kutozwa kwa, na malipo kukusanywa kutoka kwa wahusika wengine kama kampuni ya bima. Kwa mfano, tungependa kutoa maelezo ya mpango wako wa afya kuhusu ushauri uliopokea katika uwakala ili mpango wako wa afya utatulipa au kukufidia kwa

kipindi cha ushauri. Pia tunaweza kufafanua mpango wako wa afya kuhusu matibabu utakayopokea ili kupata kabla ya uidhinishaji au kuthibitisha iwapo mpango wako utashughulikia huduma / matibabu. Tutakuomba utie saini kwenye fomu ya ridhaa ili kuturuhusu kulipisha kampuni yako ya bima kwa matibabu ya matatizo ya utumiaji dawa za kulevya yaliyotolewa.

**Kwa Uendeshaji wa Utunzaji wa Afya**. Tunaweza kutumia na kutoa taarifa zako za afya kwa ajili ya uendeshaji wa uwakala. Matumizi na ufichuzi huu ni muhimu ili kuendesha uwakala na kuhakikisha kuwa watu wote wanaopokea huduma kutoka kwetu wanapokea utunzaji bora. Kwa mfano, tunaweza kutumia maelezo ya afya ili kukagua matibabu na huduma zetu na kutathmini utendakazi wa watumishi wetu katika kukuhudumia. Pia tunaweza kuchanganya maelezo ya afya kuhusu wateja wengi ili kuamua ni huduma zipi za ziada tunazofaa kutoa, ni huduma zipi zisizohitajika, na iwapo matibabu mengine mapya yanatekelezwa. Pia tunaweza kufichua maelezo kwa madaktari, wauguzi, watabibu, wasimamizi wa kesi, wafanyakazi wanafunzi na wafanyakazi wengine wa Howard Center kwa malengo ya ukaguzi na mafunzo.

Pia tunaweza kuchanganya taarifa ya afya tuliyonayo na taarifa ya afya kutoka kwa mashirika mengine ya kutoa huduma ili kulinganisha jinsi tunavyoendelea na kuona ni wapi tunaweza kuboresha katika huduma tunazotoa. Tutaondoa maelezo yanayokubainisha kutoka kwenye seti hii ya maelezo ya afya ili wengine waweze kuyatumia kujifunza utunzaji wa afya na utoaji wa utunzaji bila kujua watejamahsusi. Ili kufanikisha mapitio haya, tunatoa taarifa kwenye hifadhi ya taarifa inayoendeshwa chini ya Makubaliano ya Ushirikiano wa Kibiashara na Mtandao wa Huduma wa Vermont ili kulinda faragha ya taarifa.

Howard Center ni shirika la watoa huduma ambalo hufanya kandarasi na Jimbo la Vermont ili kutoa huduma ambazo zinaweza kujumuisha huduma za afya ya akili kwa jumuiya, huduma za ulemavu wa maendeleo na huduma za matatizo ya matumizi ya dawa na inawajibika chini ya mikataba yetu na idara mbalimbali ndani ya Wakala wa Huduma za Kibinadamu wa Vermont (“AHS”) kutoa huduma hizo. Kutokana na hayo, Idara hizi zinaweza kufikia maelezo ya afya yanayohusiana na huduma hizi za kandarasi kwa lengo la kupata matibabu kwa wateja, kufanya malipo au kwa uendeshaji wake wa huduma za afya. Aidha, tunaweza kutoa taarifa za afya kwa AHS kwa wateja ambaohawalipiwi na jimbo kulingana na Makubaliano kuweka ukomo wa matumizi ya utoaji wa tarifa za demografía na zisizo za afya kwa ajili ya uendeshaji wa huduma za afya za AHS na kwa madhumuni ya usimamizi wa afya.

**Vikumbusho vya Miadi.** Tunaweza kutumia na kufichua maelezo ili kuwasiliana nawe kama kikumbusho kuwa una miadi.

**Matibabu na Faida na Huduma Mbadala**. Tunaweza kutumia na kufichua maelezo kukuhusu ili kupata na kukupendekezea machaguo mengine ya matibabu na huduma zinazopatikana na vile vile faida na huduma nyingine zinazohusiana na afya.

**Shughuli za Kuchangisha Pesa**. Endapo tutahitaji maelezo kukuhusu au pale ambapo kushiriki kwakokunahitajika kwa shughuli za kuchangisha pesa za uwakala, uwakala utapata idhini yako. Hakuna maelezo yatakayotolewa kwa lengo hili bila idhini yako ya maandishi.

**Utafiti.** Katika hali maalum, tunaweza kutumia na kufichua maelezo ya afya kwa malengo ya utafiti. Kwa mfano, mradi wa utafiti unaweza kujumuisha ulinganishaji wa afya na afueni ya wateja wote waliopokea awamu moja ya matibabu ikilinganishwa na wale waliopokea nyingine, kwa hali sawa. Miradi yote ya utafiti sharti ipitie mchakato maalum wa uidhinishaji. Mchakato huu hutathmini mradi uliopendekezwa wa utafiti na matumizi yake ya maelezo ya afya, ukijaribu kusawazisha mahitaji ya utafiti na mahitaji ya wateja kutaka ufaragha wa maelezo yao ya afya. Kabla tutumie au kufichua maelezo ya afya kwa utafiti, mradi utakuwa umeidhinishwa kupitia mchakato huu wa uidhinishaji utafiti. Tunaweza, hata hivyo,

kufichua maelezo ya afya kukuhusu kwa watu wanaojiandaa kufanya mradi wa utafiti; kwa mfano, kuwasaidia kutafuta wateja walio na mahitaji maalum ya afya, maadammaelezo ya afya wanayokagua yasiende kinyume na uwakala. Kila wakati tutakuomba idhini maalum iwapo mtafiti atakia jina, anwani na maelezo yako mengine yanayokutambulisha, au atahusishwa katika utunzaji wako katika uwakala.

**<u>Inavyohitajika Kisheria</u>**. Tutafichua maelezo yako ya afya tukihitajika kufanya hivyo na shirikisho, taifa au sheria ya ndani. Katika Mermont, hii itajumuisha wathiriwa wa unyanyasaji wa watoto; kutelekezwa au kuwatumia vibaya watu walio katika mazingira magumu; au wakati ambapo mtoto aliye chini ya umri wa miaka kumi na sita ni mwathiriwa wa uhalifu; na majera yaliyotokana na risasi. Kutokana na hali mahsusi, Idara zilizo katika Uwakala wa Vermont wa Huduma za Binadamu tunaoshirikiana wamewezeshwa kufikia maelezo ya afya ili kutekeleza majukumu yao. Tunahitajika kufichua maelezo yako ya afya kwako na kwa yeyote utakayeomba kwa idhinisho la maandishi kuyapokea.

**<u>Kuzuia Tishio Hatari na Kubwa kwa Afya au Usalama</u>**. Tunaweza kutumia na kufichua maelezo yako ya afya yakihitajika ili kuzuia tishio hatari kwa afya na usalama wako au hatari kuu kwa mtu anayetambulika au kundi la watu. Ufichuzi wowote, hata hivyo, utakuwa tu kwa mtu anayeaminika kwa kweli kuwa anaweza kusaidia kuzuia tishio.

<u>HALI MAALUM</u>

**<u>Jeshi na Maveterani</u>**. Kama wewe ni mwanajeshi, tutaweza kutoa maelezo ya afya yanayokuhusu kama inavyohitajika na mamlaka ya amri jeshi.

**<u>Fidia kwa Wafanyakazi</u>**. Tunaweza kutoa maelezo ya afya yanayokuhusu kama inavyoisdhinishwa na fidia kwa wafanyakazi au programu kama hizo kama inavyoidhinishwa na sheria ya Vermont. Programu hizi hutoa faida kwa majeraha au magonjwa yanayotokana na kazi.

**<u>Hatari za Afya ya Umma</u>**. Tunaweza kufichua maelezo ya afya kukuhusu kwa shughuli za afya ya umma. Shughuli hizi ni pamoja na zifuatazo:

- Kuzuia au kudhibiti ugonjwa, jeraha au ulemavu;
- Kuripoti vifo;
- Kuripoti unyanyasaji wa watoto au utelekezaji;
- Kuripoti matumizi mabaya, utelekezaji au kutumia vibaya watu walio katika mazingira magumu; kushukiwa kwokote kwa unyanyasaji, utelekezaji, au unyanyasaji wa wakongwe (umri wa 60 au zaidi), au mtu mzima mlemavu aliye na matatizo ya kimwili au kiakili, kunafaa kuripotiwa;
- Kuripoti athari ya matibabu au matatizo ya bidhaa;
- Kuwaarifu watu kuhusu usitishaji wa bidhaa ambazo huenda wanazitumia;
- Kumwarifu mtu ambaye huenda ameambukizwa ugonjwa au anaweza kuwa na hatari ya kuambukizwa au kueneza hali au ugonjwa wa maambukizi

**<u>Shughuli za Usimamizi wa Afya</u>**. Tunaweza kutoa taarifa ya afya kwa shirika usimamizi wa afya, kama vile Idara za Shirika la Huduma za Binadamu la Vermont ya Afya ya Akili, Ulemavu ya Wazee na Kuishi kwa Kujitegemea na Afya ambao tumekuwa na mkataba nao, kwa shughuli zilizoidhinishwa kisheria. Shughuli hizi za uangalizi ni pamoja na, lakini haziishii tu katika, ukaguzi, uchunguzi, peksheni, na utoaji leseni. Shughuli hizi ni muhimu kwa serikali kuchunguza mfumo wa utunzaji wa afya, mipango ya serikali, na uzingatiaji wa sheria za haki za kiraia. Tunaweza kuyafichua maelezo ya afya kukuhusu bila ya ruhusa yako kwa Katibu wa Idara ya Marekani ya Afya na Huduma za Binadamu na/ au Ofisi ya Haki za Kiraia wakati wanaandaa uhakiki wa uzingatiaji, uchunguzi au hatua ya utekelezaji au kwa minajili ya ripoti ya lazima ya ukiukaji wa maelezo ya afya.

**Utekelezaji wa Sheria.** Tunaweza kuyafichua maelezo yako ya afya kwa afisa wa utekelezaji wa sheria kwa mujibu wa sheria au kutii amri ya mahakama au kibali cha kusaka. Tunaweza pia kufichua taarifa finyu kwa afisa wa utekelezaji wa sheria ili kuripoti uhalifu uliofanywa kwenye maeneo yetu au kwa kumtambulisha mtu aliyepotea au mshukiwa wa kusaidia uchunguzi wa kihalifu.

**Migogoro na Vikao vya Kisheria**. Kama umehusishwa katika kesi au mgogoro, tunaweza kufichua maelezo ya afya kukuhusu kutokana na amri ya korti au utawala. Katika kesi fulani za kisheria, kuna taratibu mahususi ambazo tunatakiwa kufuata kabla ya rekodi za matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya kufichuliwa.

**Maafisa wa Afya ya Umma na Wakurugenzi wa Mazishi.**Tunaweza kutoa maelezo kwa afisa spesheli wa kuchunguza mambo ya vifo au mchunguzi wa matibabu. Hii inaweza kuwa muhumi, kwa mfano, ili kumtambua marehemu au kuthibitisha chanzo cha kifu. Pia tunaweza kutoa maelezo ya afya kwa wakurugenzi wa mazishi hivyo basi kuwaidhinisha kufanya shughuli zao.

**Watu Waliokizuizini**. Kama wewe ni mfungwa wa taasisi ya kurekebisha tabia au chini ya kizuizi cha afisa anayetekeleza sheria, tunaweza kutoa maelezo ya afya kukuhusu kwa taasisi ya kurekebisha tabia au afisa anayetekeleza sheria kulingana na utunzaji uliotolewa ulipokuwa kizuizini. Toleo hili linaweza kuwa muhimu (1) kwa taasisi kukutolea utunzaji wa afya; (2) kulinda afya na usalama wako au afya na usalama wa wengine; au (3) kwa usalama na ulinzi wa taasisi ya kurekebisha tabia.

**Huduma ya Afya ya Uzazi na Jinsia.** Rekodi za afya zinazohusiana na huduma ya afya ya uzazi na inayothibitisha jinsia zinalindwa na usiri wa jimbo na masharti ya sheria ya ngao.

"Huduma za afya ya uzazi" inamaanisha vifaa, matunzo na huduma zote za matibabu, afya ya tabia, afya ya akili, upasuaji, akili, matibabu, uchunguzi, uzuiaji, urekebishaji au usaidizi, ikiwa ni pamoja na dawa, zinazohusiana na ujauzito, uzazi wa mpango, usaidizi wa kuzaa, udhibiti wa kupoteza mimba, au uavyaji wa mimba.

"Huduma za afya zinazothibitisha jinsia" inamaanisha vifaa, matunzo na huduma zote za matibabu, afya ya kitabia, afya ya akili, upasuaji, akili, matibabu, uchunguzi, kinga, urekebishaji au usaidizi, ikiwa ni pamoja na dawa, zinazohusiana na matibabu ya dysphoria ya kijinsia na ukosefu wa kijinsia.

Hatutafichua rekodi kama hizo kwa matumizi katika kesi yoyote ya madai, jinai, mirathi, utawala, au sheria, wala kwa kujibu maombi kutoka kwa vyombo vya nje ya nchi—ikiwa ni pamoja na hati za wito au amri za mahakama—isipokuwa ufichuzi huo uwe (1) umeidhinishwa na wewe; (2) inavyotakiwa na Vermont au sheria ya shirikisho; au (3) kulazimishwa na amri ya mahakama ya Vermont ambayo inajumuisha kupatikana kwa sababu nzuri. Kabla ya rekodi kufichuliwa chini ya amri ya mahakama, mahakama lazima itambue waziwazi kwenye rekodi ya ushahidi kwamba kuna sababu nzuri na kubainisha rekodi zinazopaswa kufichuliwa. Vighairi vingine pekee ni kufichuliwa kwa Bodi ya Mazoezi ya Kimatibabu ya Vermont au Ofisi ya Udhibiti wa Kitaaluma kuhusiana na uchunguzi na ufichuzi wa kweli kwa Idara ya Afya ya Vermont au Idara ya Ulemavu, Uzee, na Kuishi Kujitegemea ya Vermont kuhusiana na uchunguzi wa kweli wa kituo cha afya kilicho na leseni ya Vermont.

**Mpangilio wa Huduma ya Afya iliyopangwa.**

Howard Center inashiriki katika Programu Iliyoandaliwa wa Huduma ya Afya ("OHCA") chini ya Makubaliano ya Mfumo wa Jimbo Lote la Huduma za Migogoro ya Simu ya Mkononi ("Programu ya CMCS") kati ya Counseling Service of Addison County, Inc.; Clara Martin Center, Inc.; United

Counseling Service of Bennington County, Inc.; Northwestern Counseling and Support Services, Inc.; Howard Center, Inc.; Lamoille County Mental Health Service, Inc.; Northeast Kingdom Human Services, Inc.; Rutland Mental Health Services, Inc.; Washington County Mental Health Services, Inc., na Health Care & Rehabilitation Services of Southeastern Vermont, Inc. (pamoja, "Washiriki wa Mgogoro wa Simu ya Mkononi OHCA"). Tunafanya kazi pamoja kupitia shughuli za pamoja ili kutoa huduma za dharura za simu na utendakazi saidizi ikijumuisha usimamizi wa nyenzo, kuripoti, uhakikisho wa ubora, usimamizi wa matumizi, teknolojia ya habari na malipo ili kutoa huduma za haraka za jumuiya za simu za mkononi.

Kama sehemu ya Mgogoro huu wa Simu ya Mkononi OHCA, Mshiriki wa Mgogoro wa Simu OHCA anaweza kubadilishana PHI yako inapohitajika ili kutekeleza shughuli na shughuli za pamoja za Programu ya CMCS.

Kila Mshiriki wa Mgogoro wa Simu OHCA anasalia kuwa huluki tofauti ya kisheria na anawajibika kibinafsi kutimiza wajibu wake wa kisheria chini ya HIPAA na sheria nyingine zinazotumika za faragha. Notisi hii inafafanua jinsi Howard Center na, wanapotenda kupitia Mgogoro wa Simu ya Mkononi OHCA, wanaweza kutumia na kufichua PHI yako na ni haki gani unazo kuhusu maelezo hayo. Wakati sheria zingine, kama vile sheria za usiri za afya ya akili za Vermont au 42 C.F.R. Sehemu ya 2 inayosimamia rekodi fulani za matatizo ya matumizi ya dawa, kutoa ulinzi zaidi kwa maelezo yako, Howard Center na Washiriki wa Mgogoro wa Simu ya Mkononi OHCA watafuata sheria hizo na hawatatumia au kufichua maelezo yako kwa njia ambazo sheria hizo haziruhusu.

<u>MATUMIZI YA TAARIFA YA AFYA INAYOHITAJI IDHINI YA MAANDISHI</u>

Matumizi na utoaji mwingine wa taarifa ya afya isiyoangaziwa kwenye ilani hii au sheria zinazotekelezwa kwetu yatafanyika tu kwa idhini yako ya maandishi. Mifano inaweza kujumuisha taarifa ya matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya utoaji wa taarifa kwa mawakili (isipokuwa kwa wanasheria wa Shirika hili), waajiri, Afisi ya Vermont ya Huduma za Ukakamavu wa Ulemavu au wengine unaowajua, lakini wasiohusishwa katika utunzaji wako. Pia, matumizi na ufichuzi wa maelezo ya afya kwa malengo ya mauzo, na ufichuzi ulio na mauzo ya maelezo ya afya yanahitaji uidhinishaji. Ukitupatia kibali cha kutumia au kufichua maelezo ya afya kukuhusu, unaweza kubatilisha kibali hicho, katika maandishi, wakati wowote. Ukibatilisha kibali chako, hatutaweza tena kutumia au kufichua maelezo ya afya kukuhusu kwa sababu ambazo zimeangaziwa na idhini yako ya maandishi. Unaelewa kuwa hatuwezi kuangalia tena ufichuzi wowote tumeufanya kwa kibali chako, na kuwa tunahitaji kuhifadhi rekodi zetu za huduma tuliyokutolea. Unaelewa kuwa maelezo ya afya yanayolindwa ambayo yanafichuliwa yanaweza kufichuliwa upya kwa njia ambayo haijalindwa tena na HIPAA.

**<u>Vikosi vya Afya ya Jamii (“CHT”).:</u>** Vikosi hivi viliundwa chini ya ushirika wa Vermont Blueprint for Health na vina mfumo ulioandaliwa ili kujenga ushirikiano kati ya watoaji wa huduma za afya, wenyeji na mashirika ya Serikali pamoja na mashirika yanayosaidia wanajamii yaliyojitolea kuimarisha ubora wa maisha kupitia kwa usimamizi wa huduma. Huduma hizi zinaweza kuwa za kifedha, kimwili, kihisia ama kielimu katika hali halisi. Watoa huduma wako wa afya wanaweza tu kutoa taarifa yako ya kiafya kwa CHT iwapo tu umetoa idhini kwa maandiko ya kuwaruhusu kupeana tarifa hiyo.

<u>HAKI ZAKO ZINAZOHUSIANA NA MAELEZO KUKUHUSU</u>

*Usaidizi wowote (kimwili, mawasiliano, n.k.)unataka kutekeleza haki zako utatolewa kwako na uwakala.*

Una haki zifuatazo kulingana na maelezo tunayodumisha kukuhusu:

**<u>Haki ya Kupitia na Kunakili</u>**. Una haki ya kupitia na kupata nakala ya taarifa ya afya yanayoweza kutumika kufanya uamuzi kuhusu utunzaji wako. Hii inaweza kujumuisha rekodi za afya na utozaji kwa pamoja. Tumejizatiti kujibu maombi yako ya ufikiaji wa maelezo yako ya afya haraka iwezekanavyo na bila kuchelewa kusikohitajika. Chini ya HIPAA, tunatakiwa kutoa ufikiaji wa rekodi zako ndani ya siku 30 baada ya ombi lako. Ikiwa rekodi zako hazipatikani kwa urahisi, tunaweza kuongeza muda huu hadi siku 30 zaidi, lakini tutakujulisha kwa maandishi sababu ya kuchelewa. Unaweza pia kuomba kwamba tutume rekodi zako kwa mtu mwingine au chombo unachochagua.

Ili kukagua au kupata nalaka ya maelezo ya afya, sharti uwasilishe ombi lako katika maandishi kwa daktari wako au Idara ya Maelezo ya Afya (HowardCenter, 300 Flynn Ave Burlington, VT 05401). Kama unaomba nakala ya maelezo, tunaweza kutoza ada inayoeleweka na inayotokana na gharama kwa ajili ya kunakili, kutuma barua, au vifaa vinavyohusiana na ombi lako. Kama unataka nakala ya elektoniki katika aina au umbizo maalum la rekodi yako ya afya na hatuko tayari kutoa nakala katika aina au umbizo hilo, tutafanya kazi na wewe ili kutoa aina au umbizo mbadala kwa nakala ya elektroniki.

Kuna matukio machache ambapo tunaweza kukataa ombi lako la kukagua au kupata nakala ya maelezo yako ya afya.

**<u>Haki ya Marekebisho</u>**. Ukihisi kuwa maelezo ya afya tuliyo nayo kukuhusu sio sahihi au sio kamilifu, unaweza kutuomba turekebishe maelezo. Una haki ya kuomba marekebisho maadam maelezo yanahifadhiwa na au kwa uwakala.

Ili kuomba marekebisho, lazima ombi lako lifanyike katika maandishi na kuwasilishwa kwa mwandishi wa ingizo ungependa kurekebisha au kwa Idara ya Maelezo ya Afya Department (HowardCenter, 300 Flynn Ave Burlington, VT 05401). Pia, lazima utoe sababu inayounga mkono ombi lako.

Tunaweza kukataa ombi lako kwa marekebisho iwapo haliko katika maandishi au halina sababu ya kuunga mkono ombi hilo. Pia, tunaweza kukataa ombi lako kama utatuomba kurekebisha maelezo ambayo:

- Hayakuundwa na sisi, isipokuwa mtu au shirika lililounda maelezo halipatikani tena ili kufanya marekebisho;
- Sio mojawapo ya seti ya rekodi teule iliyowekwa na au kwa uwakala;
- Sio mojawapo ya maelezo utakayoruhusiwa kukagua na kunakili; au,
- Yalithibitishwa kuwa sahihi au kamilifu na uwakala.

**<u>Haki ya Uhasibu wa Ufichuzi</u>**. Una haki ya kuomba "uhasibu wa ufichuzi." Hii ni orodha ya ufichuzi tulioufanya wa maelezo ya afya kukuhusu uliohitajika kisheria na/au haukuidhinishwa nawe. Orodha ya ufichuzi huo haitajumuisha ufichuzi uliofanywa kwa madhumuni ya matibabu, malipo ya huduma za matibabu au operesheni za utunzaji wa afya zinazohusiana na huduma za matibabu.

Ili kuomba orodha hii au uhaisbu wa ufichuzi, lazima uwasilishe ombi lako katika maandishi kwa Idara ya Maelezo ya Afya (HowardCenter, 300 Flynn Ave Burlington, VT 05401). Ombi lako lazima lionyeshe kipindi cha muda, ambacho hakistahili kuwa zaidi ya miaka sita. Ombi lako linafaa kuonyesha unahitaji orodha katika aina ipi (kwa mfano, kwenye karatasi, kielektroniki). Orodha ya kwanza uliyoomba baada ya kipindi cha miezi 12 itakuwa bila malipo. Kwa orodha za ziada, tunaweza kukutoza gharama za kutoa orodha. Tutakufahamisha kuhusu gharama zinazohusika na unaweza kuchagua kuondoa au kurekebisha ombi lako wakati huo kabla gharama zozote zitekelezwe.

**<u>Haki ya Kuomba Vikwazo</u>**. Una haki ya kuomba vikwazo au kutofikia maelezo ya afya tunayotumia au kufichua kukuhusu kwa matibabu, malipo au uendeshaji wa utunzaji wa afya. Hatuhitajiki kukubali ombi

lako isipokuwa ombi lako ni la kupunguza ufichuzi katika mpango wa afya kwa lengo la kufanya malipo au uendeshaji wa utunzaji wa afya ambao pengine hauhitajiki kisheria au mtu mwingine kwa niaba yako kando na mpango wako wa afya amelipia huduma hizo kikamilifu wakati ambapo huduma za afya zinatolewa. Hata hivyo, kama tutakubaliana nauzuiliwaji ulioombwa au uwekaji mipaka, tutazingatia ombi lako isipokuwa maelezo yanahitajika ili kukutolea matibabu ya dharura.

Pia una haki ya kuomba kiwango cha maelezo ya afya kukuhusu tunachofichua kwa mtu mwingine anayehusika katika utunzaji wako au malipo ya utunzaji wako, kama mwanafamilia. Kwa mfano, unaweza kutuomba tusitumie au kufichua maelezo kuhusu mafunzo ya ushauri uliyopokea.

Ili kuomba vikwazo, lazima ufanye ombi lako katika maandishi kwa mfanyakazi msajili au daktari wako. Katika ombi lako, lazima utuambie (1) maelezo yapi unayotaka kupunguza; (2) iwapo unataka kupunguza matumizi, ufichuzi wetu au vyote kwa pamoja; na (3) ungependa upunguzaji utekelezwe kwa nani, kwa mfano, ufichuzi kwa mke/mme wako.

**<u>Haki ya Kuomba Mawasiliano ya Siri</u>**. Una haki ya kuomba kuwa tuwasiliane nawe kuhusu masuala ya afya katika njia Fulani au katika eneo fulani. Kwa mfano, unaweza kuomba kuwa tuwasiliane nawe tu kazini au kwa barua.

Ili kuomba mawasiliano ya siri, lazima ufanye ombi katika maandishikwa mfanyakazi msajili au daktari wako. Hatutakuuliza sababu ya ombi lako. Tutashughulikia maombi yote ya kuridhisha. Ombi lako lazima libainishe jinsi au mahali ungependa kufikiwa.

**<u>Haki ya Nakala ya Karatasi ya Ilani Hii</u>**. Una haki ya nakala ya karatasi ya ilani hii. Unaweza kutuomba kukupatia nakala ya ilani ya sasa wakati wowote.

Ili kupata nakala ya karatasi ya ilani hii, wasiliana na Afisa wa Faragha waHoward Centerkwa (802) 488-6900.

**<u>Matumizi ya Akili Bandia.</u>** Programu yetu inaweza kutumia teknolojia za akili bandia (AI) kusaidia kuchanganua na kudhibiti maelezo yako ya afya ili kuboresha huduma yako na uendeshaji wa programu. Zana za AI zinapofikia maelezo yako ya afya, tunahakikisha kwamba zinafikia tu kile kinachohitajika kwa kazi iliyopo, na kwamba ulinzi wote wa faragha na usalama unaohitajika kisheria unafuatwa.

AI hutusaidia kugundua ruwaza, kuboresha ufanyaji maamuzi wa kimatibabu, na kusaidia katika kazi za usimamizi. Hata hivyo, AI haichukui nafasi ya hukumu au kufanya maamuzi ya mtoa huduma wako wa afya. Maamuzi yote ya mwisho hufanywa na mtoa huduma wako kulingana na utaalamu wao wa kitaalamu.

Matumizi ya AI yanadhibitiwa kabisa, na maelezo yako yanasalia kuwa siri kwa mujibu wa HIPAA na sheria nyingine zinazotumika.

<u>Usalama wa Maelezo ya Afya.</u>

Kuna mbinu mwafaka za usalama za kutunza na kulinda usiri wa maelezo yako ya afya. Kutokana na asili ya mazoea ya huduma za binadamu zinazolingana na jamii, waakilishi wa uwakala wanaweza kumiliki maelezo yako ya afya nje ya uwakala. Katika hali kama hizi, waakilishi wa uwakala watahakikisha usalama na usiri wa maelezo katika njia inayofikia sera ya uwakala, Taifa na Sheria ya Shirikisho.

Mabadiliko Katika Ilani Hii

Tunahifadhi haki ya kubadilisha ilani hii. Tunahifadhi haki ya kutekeleza ilani iliyobadilishwa au kurekebishwa kwa maelezo ya afya ambayo tayari tunayo kukuhusu na vile vile maelezo yoyote tutakayopokea siku zijazo. Tutachapisha nakala ya ilani ya sasa katika vituo vyote vya uwakala. Ilani itajumuisha tarehe ya kutekelezwa. Endapo tutabadilisha nyenzo katika ilani hii, tutaweza, kabla ya mabadiliko kutekelezwa kuchapisha tangazo la mabadiliko katika kila kituo cha HowardCenter.

Malalamiko

Kama unaamini haki zako za faragha zimekiukwa, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Howard Center au kwa Katibu wa Idara ya Afya na Huduma za Binadamu. Ili kuwasilisha malalamiko kwa uwakala, wasiliana na: Nambari ya Dharura ya Malalamiko kwa simu katika (802)-488-7195 au barua pepe kwa compliancecomplaint@howardcenter.org

Hutaadhibiwa kwa kuwasilisha malalamiko.

Katibu wa Idara ya Afya ya Huduma za Binadamu anaweza kufikiwa kupitia afisi yake ya eneo katika Afisi ya haki za Kiraia, Idara ya Marekani ya Afya na Huduma za Binadamu, Kituo cha Serikali, Jengo la Shirikisho la J.F. Kennedy – Chumba cha 1875, Boston, Massachusetts 02203, simu ya sauti (800) 368 1019, fax (617) 565-3809, TDD (800) 537 7697 au tuma barua pepe kwa ocrmail@hhs.gov.